**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA MAGALULA S. MAGALULA ALIYOITOA KWENYE SEMINA KUHUSU MFUMO WA RAJISI YA NAMBA ZA UTAMBULISHO WA SIMU ZA KIGANJANI MJINI SUMBAWANGA TAREHE 11 MACHI, 2016.**

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,

Viongozi kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,

Watendaji wa Serikali mliopo mahali hapa,

Watoa huduma za Mawasiliano,

Wadau wa Sekta ya Mawasiliano,

Waandishi wa Habari,
Wageni waalikwa,
**Mabibi na Mabwana**;

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa siku hii ya leo.

Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwasafirisheni salama wageni wetu kutoka Ofisi ya Mamlaka ya Mawasiliano Kanda. Mji wetu wa Sumbawanga ni tulivu ***"Karibu sana".***

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi wa Mamlaka ya Mawasiliano Kanda kwa kunialika kuwa mgeni rasmi na pia ili niweze kushiriki katika semina hii kuhusu **Mfumo wa Rajisi ya Namba za Utambulisho WA SIMU ZA KIGANJANI**.

Kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kuwapongezeni Viongozi na Watumishi wote wa TCRA kwa jithada na kuwezesha kuwekwa kwa mfumo huu wa Rajisi ya Namba za Utambulisho wa simu za Kiganjani. Itambulike kuwa kwa sasa teknolojia imekuwa ndani ya Nchi yetu na Nje ya Mipaka yetu.

Kutokana na kukuwa kwa teknolojia pia vitendo vya uhalifu vimeongezeka, hapa kwetu Tanzania vitendo hivyo vimeweza kudhibitiwa kutokana na kazi nzuri inayofanywa na TCRA. Jambo hilo ni zuri kwa usalama wa Nchi na wote wanaotumia huduma na bidhaa za mawasiliano

**Ndugu Washiriki Mabibi na Mabwana;**

Sote tunatambua kwa kipindi tulichopo sasa ni kwa kiwango gani sekta ya Mawasiliano nchini imeweza kupiga hatua ukilinganisha na miaka michache nyuma, mafanikio haya ya kukua kwa Sekta ya mawasiliano yanatokana na ushirikino uliopo miongoni mwa Wadau wa mawasiliano na Mamlaka ya mawasiliano Tanzania. Kama Serikali tunaipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuwezesha kukua kwa Sekta ya mawasiliano katika kasi ambayo tunaishuhudia sasa.

Ukiitazama Sekta ya mawasiliano kwa upana wake utagundua kuwa ni kichocheo kikubwa cha maendeleo yanayoenda sambamba na ukuwaji wa teknolojia katika. Mbali na kutoa ajira kutokana na idadi kubwa ya Wananchi wanaoshiriki kama Wadau katika Sekta ya Mawasiliano, lakini pia katika miaka ya

hivi karibuni makampuni ya mawasiliano yanatoa huduma za kibenki, kulipia bili za maji na umeme, kusafirisha fedha, kupata taarifa za michezo, kuuza na kununua bidhaa, taarifa za kibiashara na nyingine nyingi. Hii inaonyesha kuwa sekta ya mawasiliano imekuwa na ni chachu ya maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na kwa taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na TCRA zinaonyesha kuwa sekta ya Mawasiliano imeendelea kuimarika kwa kiwango cha kikubwa. Ni matumaini yangu kwamba endapo tutaendelea kuboresha mazingira yetu na usimamizi bora, tutazidi kuvutia wawekezaji wengi zaidi ili kupanua mtandao wa mawasiliano hadi vijijini na hivyo kuhakikisha kuwa maeneo yote ya nchi yetu yakiwemo yale ya vijijini yanapata huduma zote za msingi za mawasiliano ya simu, posta na utangazaji. Laini za simu zaidi ya **milioni 36** sio jambo  dogo. Mawasiliano kwa njia ya simu ya mkononi yameongeza mzunguko wa biashara kwa kuwa kiunganishi baina ya muuzaji na mnunuaji kwa kujua hali ya soko na bei za bidhaa hata kabla ya pande hizo mbili kukutana.

**Ndugu Washiriki Mabibi na Mabwana;**

Maendeleo katika sekta ya mawasiliano nchini hayakutokea kwa bahati mbaya, bali ni jitihada za makusudi na uwepo sera bora, sheria madhubuti zinazoenda na wakati, kanuni mahiri na mfumo wa leseni kama ule wa muingiliano wa tekinolojia kama alivyoeleza Mkurugenzi Mkuu hivi punde.

Hali kadhalika nchi yetu ina sheria za mawasiliano zinazokwenda na wakati ikizingatiwa kuwa sekta ya mawasiliano na teknologia vinakuwa kwa kasi sana.

**Ndugu washiriki Mabibi na Mabwana;**

Japokuwa inaweza kuwa ngumu kutaja majina ya makampuni yaliyowekeza hapa nchini. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati kwa hatua yao ya kuwekeza, uamuzi huo umesaidia kukua kwa sekta ya mawasiliano na kuboresha njia za mawasiliano. Uwingi wadau wa Mawasiliano umepelekea kupungua kwa gharama za mawasiliano ya simu na utangazaji. Hali ambayo inaenda sambamba na kuongezeka kwa pato la Taifa.

Wito wangu kwa Wadau wa Sekta ya mawasiliano ni vema kutumia vizuri fursa iliyopo kwa kuwekeza zaidi katika Sekta ya Mawasiliano. Tanzania ni nchi ya amani na yenye utulivu mkubwa, Serikali inaweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza Sekta hii ya Mawasiliano, pia Serikali imewekeza kwa kujenga miundombinu ya Mawasiliano. Fursa hiyo ni vema ikachangamkiwa.

**Ndugu washiriki Mabibi na Mabwana;**

Pamoja na faida kubwa ambayo tunaishuhudia ya kukua kwa Sekta ya mawasiliano, kuna baadhi ya changamoto ambazo zinatakiwa kushughulikiwa kwa kuwa ni doa katika maendeleo ya Sekta hii.

Wapo baadhi ya watu ambao kwa makusudi wanatumia isivyo Sekta ya Mawasiliano kinyume na utaratibu na kinyume cha sheria. Kuna wimbi la watu ambao wanatumia fursa ya uwepo na ustawi wa Sekta ya Mawasiliano kwa kufanya vitendo vya uhalifu na utapeli. Jambo hili siyo zuri na halivumiliki. Mamlaka ya Mawasiliano kama jicho letu mnawajibu wa kubaini hawa wachache wanaofanya vitendo hivyo ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Wapo watu wanaotumia vibaya Sekta ya Mawasiliano badala ya kujiletea maendeleo wao wanatumia Sekta hii kukejeli na kutukana na kuweka picha zisizo na maadili hususani kupitia mitamdao ya kijamii ( social media).

Serikali kupiia vyombo vya usalama imekuwa inasimamia Sheria hizi. Kwa kiasi kikubwa tumeweza kuwahakikishia wananchi usalama wao wanapotumia mitandao ya mawasiliano. Sheria ya Mawasiliano na Kielektrioniki na Posta ya 2010, Sheria ya Makosa ya Mtandao - Cyber Crimes Act ya 2015 na Kanuni mbalimbali kwa pamoja vilitungwa kumlinda mwananchi.

Hatua za kiusimamizi *(regulatory interventions)* kama hii ya kuwa na Mfumo wa Rajisi ya Namba za Utambulisho wa simu za kiganjani, ni muhimu katika kuweka mazingira mazuri ya matumizi ya huduma na bidhaa za mawasiliano zikiwemo simu zenyewe za kiganjani.

Nimeambiwa pia kwamba Mfumo huu wa Rajisi ya Namba za Utambulisho wa simu za kiganjani umeunganisha mifumo ya ndani ya kampuni za simu, na ili mfumo huu ufanye kazi kampuni za simu ilibidi ziwekeze kwenye kuboresha mifumo yao ili iweze kuwasiliana na Mfumo huu mkuu. Nawapongeza sana wawekezaji ambao wanatii sheria na matakwa ya nchi nia yetu ikiwa ni kuhakikisha huduma bora kabisa zinawafikia wananchi wote.

Mfumo huu wa kisasa una faida kuu mbili; **Mosi** ni Kuongeza usalama mtandaoni kwa watumiaji wa simu, kwani simu zote zitakuwa zinatambulika; **Pili** ni kuzuia matumizi ya simu zisizokuwa na viwango hivyo kuhakikisha kwamba simu zinazotumika Tanzania zina ubora stahiki. Hii pia itatoa fursa kwa wateja wa simu za kiganjani kupata bidhaa inayolingana na pesa walizotoa kununulia simu hizo (value for money).

**Ndugu washiriki Mabibi na Mabwana;**

Nimeambiwa kuwa mfumo huu utawezesha Mteja/mtumiaji wa simu kuwa na uwezo wa kuripoti mara simu yake inapoibiwa na kuifanya isiweze kutumika katika mtandao wowote wa simu hapa nchini. Hii itapunguza wizi wa simu kwani hazitakuwa na thamani ya kununulika.

Napenda kuhitimisha kwa kwa kusema kuwa ni jambo zuri kwamba leo nimezindua Mfumo huu wa rajisi ya namba za utambulisho wa simu za kiganjani. Sisi Viongozi wa Mkoa wa Rukwa tupo tayari kutoa ushirikiano ili tusibaki dunia ya peke

yetu bali tuweze kwenda pamoja kama Taifa kwa maendeleo yetu.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Magalula S. Magalula

**MKUU WA MKOA**

**RUKWA**